

## Mafuriko

Wakati wa mafuriko, maji hutiririka kwenye ardhi kavu. Wewe, nyumba yako, na vitu vyako huenda vikaharibiwa na maji. Fuata maelekezo haya ili uwe salama.

Kwa usaidizi au maelezo, dayo 2-1-1 kwenye simu yako na useme lugha yako. Kuna mtu atakaye kusaidia na maswali yako kwa lugha yako.

*Hadhari ya Mafuriko* humaanisha kunaweza kuwa na mafuriko katika eneo lako.

*Ilani ya Mafuriko* humaanisha mafuriko yako karibu kutokea au yanatokea mahali pengine.

### Sikiliza redio.

- Sikiliza stesheni ya redio ya \_\_\_\_\_ kwa maelezo ya lugha yako. Endelea kusikiliza mpaka usikie lugha yako ili ujue kinachoendelea na unachopaswa kufanyana. – AU –
- Kuwa na mtu anayeelewa Kiingereza asikilize redio ili ajue kinachoendelea na unachopaswa kufanya.

### Jitayarishe.

- Kama uko na simu ya mkononi, ichaji kabisa.
- Kama unaishi karibu na mto au kijito au kando ya ufukwe wa bahari, hamisha vitu muhimu kwenye ghorofa za juu za nyumba yako. Ingiza vitu vya nje ndani kama vile baiskeli.
- Jaza hodhi, sinki na jagi na maji. Maji haya yanaweza kutumiwa kwa kukunywa, kuoga au kuosha choo.
- Kaa ndani ya nyumba isipokuwa unapoambiwa utoke. Ukiambiwa utoke, enda sehemu iliyojuu. Kaa mbali na mito na vijito.

### Kuwa salama wakati wa mafuriko.

#### Nyumbani:

- Kama kuna maji yanayokaribia nyumba yako, usisubiri – toka na uende sehemu iliyojuu.
- Kama uligusa maji ya mafuriko, osha mikono yako na sabuni na maji masafi yaliyomoto.
- Usikule au kunywa kitu chochote kilichogusa maji ya mafuriko.
- Kama unahitaji kuenda kwa kimbilio, dayo 2-1-1 kwenye simu yako na useme lugha yako.
- Kama nyumba yako imefurika, huenda isiwe salama kurudi mpaka ikaguliwe na maofisa.

#### Nje:

- Kaa mbali na maji ya mafuriko. Maji yanaweza kuwa na uketo na yanaweza kupanda kwa haraka.
- Usitembee katika maji ya mafuriko. Hata maji ambayo hayana uketo yanaweza kusonga kwa kasi na kuwa hatari.
- Ukisikia maji, geuka na upitie njia ingine.
- Kaa mbali na nyaya za umeme zilizoanguka. Umeme unaweza kusafiri kupitia maji na kukudhuru au kukuua.
- Usiingie ndani ya nyumba zilizofurika isipokuwa wakati uko na uhakika kwamba umeme umezimwa.

#### Ndani ya gari:

- Kama lazima uendeshe gari, tumia barabara zilizosalama pekee.
- Usiendeshe gari karibu na vuzuizi.
- Usitumie barabara ambazo zimewekwa alama kwamba zimefungwa.

- Usiendeshe kwenye maji ya mafuriko. Hata maji yasiyokuwa na uketo yanaweza kuinua gari.
- Gari lako likizima mahali penye maji, toka nje ya gari na uende sehemu iliyojuu.
- Usiendeshe gari usiku wakati ni vigumu kuona.

Mafuriko • Kiingereza • Mei 2012